

**Transcript- Ibilisi wa mtu ni mtu.**

- Abdala: Karibu sana bwana.
- Joho: Asante.
- Abdala: Jisikie upo nyumbani.
- Joho: Sawasawa kabisa, asante sana.
- Vipi mbona simuoni shemeji?
- Abdala: Ah! Shemeji yupo tuu (Akiita) Zainabuu?
- Zainabu: Bee, mume wangu, umesharudi?
- Abdala: Ndiyo nimerudi, hebu njoo basi nimerudi nipo na rafiki yangu.
- Zainabu: Haya nakuja.
- Za saa hizi shemeji?
- Abdala: Nzuri tuu shemeji!
- Zainabu: Karibu sana shemeji.
- Joho: Asante sana shemeji.
- Abdala: Huyu ni rafiki yangu wa siku nyingi sana.
- Zainabu: Ah! Karibu sana.
- Joho: Asante sana.
- Abdala: Yaani tumekaa naye muda mrefu, tumejepata naye shida sana, yaani tupo naye pamoja, yaani yaani ukiniona mimi ni sawasawa na rafiki yangu, yaani ni rafiki yangu kweli.
- Zainabu: Sasa mume wangu ngoja nimuandalie mgeni chai.
- Abdala: Sawa mke wangu, yaani huyu mke wangu anajua kupika kweli, anajua kuangalia mandhari ya nyumba sana yaani kila kitu.

- Joho: Naona kweli!
- Abdala: Yaani chakula chake ni kitamu sana yaani ukionja utakipenda.
- Joho: AH! Kweli kabisa.
- Zainabu: Karibuni chai jamani.
- Wote: Asante sana.
- Zainabu: karibu sana shemeji, kunywa chai usiogope.
- Joho: Sawa shemeji, asante.
- Abdala: Yaani, chai ni tamu sana.
- Joho: Kweli kabisa ni tamu sana.
- Abdala: Yaani, nilikuambia mke wangu anajua kupika sana.  
yaani angalia mwenyewe nilivyochukua kitu,  
unaona mke wangu alivyo mzuri?
- Joho: Kweli kabisa nimeona, mke mzuri huyo!
- Abdala: Hehee! Umeona yaani nimepata kweli.
- Joho: Itabidi na mimi nijitahidi nitafute wa kwangu kama wa kwako, hongera sana.
- Abdala: Asante sana.
- Joho: Yaani hujakosea kabisa ulikaa ukafikiri na kutafuta.
- Abadala: Haya bwana asante, sasa ngoja nimalize chai tuende.
- Joho: Shemeji nashukuru sana kwa chai.
- Zainabu: Asante sana, karibu tena.
- Abdala: Sasa mke wangu mimi nataka kutoka na rafiki yangu, naona kijasho kimemtoka.

- Zainabu: Haya.
- Abdala: Ngoja mimi niende na rafiki yangu,hapo nje kucheza bao, chakula kikiwa tayari nitakuja kula.
- Zainabu: Ukirudi utakuta chakula tayari.
- Abdala: Sawa mke wangu.
- Zainabu: Karibu sana shemeji.
- Joho: Asante sana shemeji.
- Zainabu: Usiache kuja shemeji.
- Joho: Ah! Mimi shemeji nitakuja tuu.

*Baada ya wiki moja;*

- Joho: Hodi huku!
- Zainabu: Karibu shemeji, za huko?
- Joho: Nzuri tuu shemeji.
- Zainabu: Karibu sana shemeji.
- Joho: Asante sana.
- Zainabu: Za nyumbani?
- Joho: Huko salama tuu.  
Shemeji, huyu bwana nimemkuta?
- Zainabu: Hapana kaenda kazini.
- Joho: Mbona nimetoka huko kazini sijamuona?
- Zainabu: Hujamwona huko kazini kweli?
- Joho: Usikute shemeji umemficha huko ndani na hii  
baridi shemeji!
- Zainabu: Sasa shemeji nikimficha ndani tutakula nini?
- Joho: Mimi sikai sana shemeji nataka kutoka
- Zainabu: Ngoja nikuandalie chai basi.
- Joho: Hapana shemeji nitakunywa chai siku  
nyingine, lakini nina pesa kidogo hapa sasa hii  
pesa chukua itakusaidia.
- Zainabu: Asante sana shemeji.
- Joho: Hizo nywele itabidi uende saloni ili ukae vizuri  
utengenezwe vizuri, na pia unununue vipodozi  
vyako ili upendeze.

Zainabu: Asante sana shemeji.

Joho: Hata yule mzee akikuona anakusahau!

Zainabu: Haya shemeji asante, lakini una utani shemeji.

Joho: Mimi mwenyewe nikija nafurahi shemeji.

Zainabu: Sawa shemeji asante.

*Wakiwa Sokoni*

Kuluthum: Hii batiki naona kama nzuri.

Zainabu: Hah! Mimi hata sikufurahishwa nayo!

Kuluthum: Lakini ni nzuri.

Zainabu: Mimi naona hii nyeupe ni nzuri.

Kuluthum: Haya! Chagua nyengine basi.

Zainabu: Shoga kuna kitu nataka nikuambie.

Kuluthum: Kitu gani?

Zainabu: Si unamjua yule rafiki wa mume wangu?

Kuluthum: Ndiyo namjua.

Zainabu: Mimi hata simuelewi.

Kuluthumu: Kwanini?

Zainabu: Yaani jana kaja kaniletea hela, na juzi kaja kaniletea hereni, sasa unanishauri nini shoga yangu?

Kuluthum: Sasa kakuletea kivipi?

Zainabu: Mimi hata simuelewi!

Kuluthum: Amekupa kama zawadi?

- Zainabu: Mimi hata sijui, maana sielewi kama amenipa tuu au viper?
- Kuluthum: Atakuwa amekupa kama zawadi tuu.
- Zainabu: Mimi hata simuelewi.
- Kuluthum: Sasa si upokee tuu!
- Zainabu: Mimi namwogopa mume wangu.
- Kuluthum: Pokea tuu zawadi unachunga tuu ili mume wako asijue.
- Zainabu: Haya! Lakini shoga hili bazee ni zuri  
 (Mitaani, mume wa zainabu akiwa anapita)
- Jirani: Jirani habari za sasa hizi?
- Abdala: Nzuri tuu jirani.
- Jirani: Habari za nyumbani?
- Abdala: Nzuri tuu.
- Jirani: Nafuu nimekuona jirani, mbona huonekani jirani?
- Abdala: Nipo tuu jirani, shughuli nyingi.
- Jirani: Kuna kitu nataka nikuulize!
- Abdala: Kitu gani hicho?
- Jirani: Mbona ukiwa haupo yule rafiki yako anakuja nyumbani?
- Abdala: Hah! Huyo ni rafiki yangu sana wala hamna wasiwasi, ni rafiki yangu wa siku nyingi yaani tumeshibana wala hamna wasiwasi, maana hata akifika nyumbani kwangu ni sawa na kwake, na kwake ni kwangu.
- Jirani: Hamna shida kabisa.

Abdala: Kweli kabisa, sawa bwana lakini uangalie bwana!

Abdala: Haya bwana.

Jirani: Asante sana.

Haya bwana.

*Huku nyuma*

Joho: Hodi hapa!

Zainabu: Karibu shemeji.

Joho: Asante shemeji, Ah! Shemeji ngoja nikae na wewe hapa karibu.

Zainabu: Haya karibu ukae.

Joho: Shemeji nimekuletea kanga leo.

Zainabu: Ah! Asante sana shemeji yangu nimeamini unanipenda.

Abdala: Ala! Yaani unanisaliti mimi?

Zainabu: Hapana nisamehe mume wangu.

Abdala: Yaani rafiki yangu wa zamani leo unanifanyia kitendo kama hiki?

Joho: Nisamehe mzee, shetani kanipitia.

Zainabu: Nisamehe mume wangu.

Joho: Yaani mke wangu nilikuamini sana! Leo unakuja kunifanyia kitendo kama hiki.

Zainabu: Umekosa nini mke wangu? kila kitu nakupa, chakula nakupa, viatu nakupa.

Nisamehe mume wangu ni shetani tuu amenipitia.

Zainabu:

Joho: Nisamehe mzee.

Abdala: Kweli ibilisi wa mtu ni mtu!

### Vocabulary

- Mandhari- Scene

- Vipodozi- Make up